

## MUONGOZO KWA MGONJWA ALIYEKATWA KIUNGO



1. Mgonjwa yoyote aliyekatwa mguu kutokana na maradhi au kwa ajali atalazimika kusajiliwa katika kitabu cha orodha ya wagonjwa wanaohitaji kutengenezwa miguu ya bandia katika kitengo cha Orthopedic Workshop – Mnazi Mmoja Hospital. Kwa mgonjwa ambao amekatwa mguu akiwa wadini atalazimika kuripoti kitengo cha Orthopedic Workshop siku ya kuruhusiwa kutoka hospitali.
2. Pamoja na ushauri wa kitaalam ambao mgonjwa atapatiwa, kwanza atatakiwa kutoa maelezo yafuatayo:-
  - Jina kamili
  - Umri
  - Namba ya simu
  - Tarehe aliyokatwa mguu
  - Tarehe aliyoruhusiwa kutoka hospitali
  - Sababu ya kutakwa mguu.
3. Baada ya kutoa maelezo haya mgonjwa atapatiwa ushauri unaostahili juu ya uwezekano wa kutengenezwa mguu bandia na namna ya kuitunza sehemu ya mguu uliokatwa ili kumrahisishia daktari kufanya vipimo kwa ajili ya kutengeneza mguu bandia wakati utakapofika.
4. Mgonjwa atashauriwa na kufundishwa namna ya kufunga Creepe bandage kwenye sehemu ya mguu uliokatwa ili kuzuia uvimbe na kufanya sehemu iliyokatwa kuwa katika hali iliyo bora kwa utengenezaji wa mguu bandia.



5. Sehemu iliokatwa inaweza kuanza kufungwa kwa creepe bandage mara baada ya kidonda kupona vizuri , aghlabu baada ya wiki 4 au 6 toka siku sehemu ya mguu ilipokatwa.
6. Mgonjwa ataendelea kufunga creepe bandage mpaka siku ya kufanyiwa vipimo kwa ajili ya kutengenezwa mguu bandia ambapo katika hali ya kawaida vipimo vinaweza kufanywa kwa kipindi cha miezi 4 hadi 6 tokea tarehe ambayo mguu ulikatwa.



## MAFANIKIO YA VIUNGO BANDI



Hakutakuwa na tafauti kubwa na kiungo cha kimaumbile wakati wa matumizi ya viungo bandia

## KUMBUKA

Kupoteza kiungo sio sababu ya kushindwa kuendelea na shughuli zako ulizokuwa ukifanya kabla ya kupoteza kiungo hicho,

Kwa maelezo zaidi fika Kitengo cha Orthopedic Workshop Mnazi Mmoja Hospital au piga simu nambari 0773 888 454 / 0714 801724 wakati wa saa za kazi kuanzia Jumaatatu hadi Ijumaa.



ZanzibarOutreachProgram

**Zanzibar Outreach Program  
Huleta Huduma Kwa Jamii**

**MATIBABU YA MGUU RUNGU  
NA VIUNGO BANDIA**



*Imetolewa na:*

*Zanzibar Outreach Program (ZOP)  
P.O.BOX 4199*

*Zanzibar*

*Tel: 0773047979*

*Email: [zanzibaroutreach@gmail.com](mailto:zanzibaroutreach@gmail.com)*

*Ofisi zetu zipo:*

*Chumba Na. 38, Ghorofa ya pili,  
Atrahma Hospital  
Zanzibar*

## MATIBABU YA MGUU RUNGU

Matibabu ya watoto wenye miguu rungu yamegawika katika sehemu tatu kubwa, nazo ni:

### 1. Manipulation and POP Casting

- Hii ni hatua ya awali ambapo mtoto ambaye amezaliwa na matatizo ya mguu rungu huanza kupatiwa matibabu kwa kunyoosha na kufungwa POP katika miguu/mguu uliopinda.
- Kipindi kizuri kuanza matibabu ni kati ya siku 7 au 10 toka mtoto kuzaliwa.
- POP iliyofungwa inatakiwa kubadilishwa kila baada ya siku 7.
- Mtoto ataendelea kufunga POP kwa kipindi cha wiki 5 au 6 na baada ya hapo atachunguzwa na daktari hatua na maendeleo ya matibabu yaliyofikiwa.



2. Baada ya kuchunzwa mtoto ambaye amebainika matibabu yake yanahitaji matibabu ya ziada, atafanyiwa upasuaji mdogo ili kunyoosha sehemu ya kisigino iweze kukanyaga vizuri.

### 3. Utumiaji wa viatu maalum "Foot Abduction Brace"



#### INDHARI:

- Mzazi wa mtoto mwenye miguu rungu ni lazima azingatie yafuatayo:-
  1. Viatu hivi ni maalum kwa ajili ya hatua ya tatu na ni muhimu kwa mtoto mwenye miguu rungu.
  2. Ni muhimu kufuata maelezo ya daktari juu ya namna bora na sahihi ya matumizi na uvalishaji wa viatu hivi.
  3. Ili viatu viweze kufanya tiba iliyokusudiwa ni lazima viunganishwe na chuma ulichopewa baada ya kumvalisha .
  4. Kwa miezi 3 ya mwanzo mzazi atalazimika kumvalisha viatu hivi mtoto wake takriban masaa yote kwa siku hususan anapolala usiku na mchana anaweza kumpangia masaa na muda wa kumvalisha.
  5. Muda wa matumizi wa viatu hivi unaweza kupungua kadri mtoto anavyokua na kupata maelezo ya daktari.
  6. Mzazi atalazimika kumrejsha mtoto kliniki kila baada ya mwezi mmoja.

- Muda huu unaweza kubadilika kadri mtoto anavyokua na kuonesha ishara nzuri ya mafanikio ya matibabu ya mguu rungu yaliyofikiwa na kupangiwa kuonwa kila baada ya miezi 3 au 6.
- Mguu rungu unatibika! Ili kupata mafanikio ya tiba ya mguu rungu wa mtoto wako ni muhimu kwa mzazi kufuata maelekezo na masharti kutoka kwa daktari na pale ambapo una mahitaji maalum fika katika kliniki ya watoto wenye miguu rungu Mnazi Mmoja Hospital au piga simu nambari 0773 888 454 / 0714 801724 wakati wa saa za kazi Jumaatatu hadi Ijumaa.

## MAFANIKIO YA MATIBABU YA MGUU RUGU



Mafanikio kama haya hupatikana kwa kufata kiusahihi maelekezo ya daktari wakati wa matibabu